
African Centre for School Leadership

Uongozi Unaobadilisha: Namna Kisimiri ilivyoweza kuwa Shule Bora Tanzania

Makala

Novemba 2025



Waandishi: Sylvia Thuku, Benjamini Masebo, Leila Abdullahi, Edmund Aalangdong, na Caren Namalenya

The African Centre for School Leadership is a coalition of partners in Africa coordinated by:

ADEA Association for the Development of Education in Africa

ESSA Education Sub Saharan Africa

vvob education for development

Utangulizi

Katika eneo la Kusini mwa Jangwa la Sahara ubora wa uongozi shuleni umejitokeza kuwa mojawapo ya mambo muhimu katika kuboresha na kuimarisha mifumo ya elimu shuleni[1]. Wakati upatikanaji wa elimu umeongezeka kwa kiasi kikubwa, shule nyingi hasa zile za vijijini au maeneo yasiyo na huduma za kutosha bado zinakabiliwa na changamoto za kimfumo: kama vile uhaba wa walimu, miundombinu duni, ari ndogo ya walimu, na mifumo dhaifu ya uwajibikaji. Katika mazingira hayo jukumu la mkuu wa shule linakwenda kuwa si uongozi tu bali ni uongozi unaoleta mabadiliko. Jukumu ambalo linabadili utamaduni wa shule, kuhamasisha jamii, na kuwapa motisha walimu pamoja na wanafunzi.

Ndani ya ajenda ya mageuzi ya elimu nchini Tanzania kipaumbele kimewekwa katika uongozi unaolenga kuboresha mafanikio shuleni[2], ambao umesisitizwa katika vipaumbele vya kitaifa kama vile Elimu ya Kujitegemea[3]. Miongozo hii inatambua kuwa uongozi bora si muhimu tu katika kuboresha matokeo ya ujifunzaji, bali pia katika kukuza dhamira maadili na maono ya pamoja ya elimu bora. Ndani ya muktadha huu mpana ndipo mfano wa Mwalimu Emmanuel Kisongo aliyekuwa Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Kisimiri na baadae kushika nafasi mbalimbali kama vile, Kaimu Mkurugenzi wa Elimu ya Sekondari katika Ofisi ya Rais TAMISEMI unajitokeza. Safari yake ya uongozi inaakisi yale ambayo yanafanywa na kutarajiwa na Africa Centre for School Leadership (ACSL) ambayo imerekodi makala hii pia ili kuonyesha yale yaliyofanywa yametokana na msukumo binafsi, maadili ya uongozi yaliyolenga mabadiliko katika shule na kuboresha mfumo wa elimu kutokana na jitihada binafsi.

ACSL inashirikiana na washirika wa ndani barani Afrika kuimarisha mifumo ya elimu ya shule kwa kukusanya takwimu ambazo zinasaidia katika kuimarisha utengenezaji/au mageuzi ya kisera pamoja na utekelezaji wake. Kwa kukusanya kuibua na kueneza makala kama hii ya shule ya Kisimiri, hii inachangia kupata uelewa wa pamoja kuhusu kile kinachofanya kazi katika uongozi wa shule na jinsi gani malengo, ambayo dhamira kubwa iko kwa mwanafunzi yanaweza kuleta matokeo yanayopimika hata katika mazingira yenye changamoto.

Education Sub-Saharan Africa (ESSA) ikiwa ni mshirika mkuu wa ACSL, inawekeza kwa namna ya kipekee katika simulizi kama ya Mwalimu Kisongo, kwa sababu simulizi hizi zinaleta katika uhalisia wa maisha dhamira ya ESSA: kutumia Ushahidi wa takwimu ili kuendelea kuboresha uboara wa elimu barani Afrika. Dhamira ya ESSA ya kutumia Ushahidi watakwimu, kuchochea ubunifu, na kutatua changamoto kulingana na mazingira husika, inaendana kabisa na jinsi Mwalimu Kisongo alivyobadilisha maono yake na kuwa matokeo kwa jamii ya shule yake kijijini iliyokumbana na changamoto kubwa.

Mazingira ya shule

Mwalimu Kisongo alisema shule ilikuwa na jumla ya walimu tisa (9) tu kwa wanafunzi 2,500 miundombinu duni, na haikuwa na sifa nzuri kitaaluma kwenye matokeo ya kitaifa. Alikuwa mkuu wa tatu tangu shule ianzishwe. Aliehamia kutoka katika shule ya mjini yenye vifaa na mazingira mazuri, Mwalimu Kisongo alikumbana na taasisi ambayo ilikuwa karibu kushindwa kufanya kazi kama shule.

Uongozi Unaoleta Mabadiliko: Mkazo kwenye Lengo Kuu: Wanafunzi Kwanza

Mwalimu Kisongo alijisemea mwenyewe kuwa ni jukumu lake kubadilisha shule kutoka “sifuri kwenda kuwa bora”. Na aligundua kuwa hakuna kilichokuwa kinawezekana kufanyika pale zaidi ya watu kusubiri miujiza kutokea. Hivyo basi aliitisha mkutano wa walimu pamoja na wanafunzi. Wanafunzi walifika lakini hakukuwa na Mwalimu hata mmoja aliefika. Hakupoteza matumaini.

[1] VVOB & UNESCO. (2021). School leadership competences in Sub-Saharan Africa
[2] Ministry of Education, Science and Technology (MoEST) (2021). Education Sector Development Plan 2021/22–2025/26
[3] Julius K. Nyerere, Education for Self-Reliance, 1967.

Kwa Pamoja na wanafunzi walijadili kwa kina mambo yanayoihusu shule yao na Tanzania kwa ujumla. Hii ikiwa ni pamoja na mstakabari wa elimu yao na sera ya elimu ya kujitegemea[4] kwa kuwaeleza nini maana ya kusimama kwa miguu yao wenyewe ili waweze kupambana katika ulimwengu wa ajira. Mazungumzo hayo yakawa nguzo kuu ya utamaduni mpya wa shule uliotegemea uelewa wa pamoja. Ingawa mwanzoni walimu walionekana kutokushiriki kikamilifu, aliendelea kusisitiza kwa kuweka mifumo ya uwajibikaji, kufundisha madarasa yeye mwenyewe, na taratibu kujenga uaminifu na dhamira ya uwajibika miongoni mwa wafanyakazi.

"Naamini mtu muhimu shuleni ni mwanafunzi. Wanajua ni kwanini wako shuleni,"

Alisema Mwalimu Kisongo.



Emmanuel Kisongo

Mbinu zake zilisimamia katika hatua mbili za uwajibikaji

1. Mabadiliko ya tamaduni na mtizamo, ambapo uwajibikaji na nidhamu viliingizwa katika utendaji wa kila siku.
2. Uboreshaji wa taaluma na taasisi, Uboreshaji wa kitaaluma na wa taasisi, uliopatikana kupitia umakini wa hatua kwa hatua na kulenga matokeo ya kidato cha nne na cha sita.

Kujenga Mazingira ya Kujifunzia

Baada ya wiki chache Mwalimu Kisongo alijikita zaidi kubadilisha mitizamo, jambo ambalo lilikuwa kipaumbele chake cha kwanza kimkakati. Alilenga kuhakikisha mazingira wezeshi ya ujifunzaji yanapatikana. Taratibu, walimu walianza kushiriki tena. Alifundisha madarasa pale palipohitajika na kupanga mifumo ili kila mtu, kuanzia wafanyakazi hadi wanafunzi, wawe na majukumu maalumu.

Kipimo cha Mabadiliko, Kitaifa

Matokeo ya uongozi wake yalibadilisha na kuwa alama. Ndani ya miaka mitatu, Kisimiri ilionyesha mabadiliko kwa kidato cha kwanza hadi cha nne, na ndani ya miezi sita (6) mabadiliko kwa kidato cha tano na cha sita yalionekana. Kutambuliwa kitaifa kulifuata: mwaka 2016 shule iliongoza katika matokeo ya mtihani wa taifa ya kidato cha sita (ACSEE), na miaka iliyofuata 2018 na mwaka 2024, iliendelea kuwa moja ya shule za umma zinazofanya vizuri nchini [5] [6].

Mabadiliko haya yameweka alama, kutoka kutojulikana hadi kutambuliwa kitaifa.

[4] Julius K. Nyerere, Education for Self-Reliance, 1967.

[5] The Citizen – Kisimiri Secondary School reveals the secret behind their performance in Form Six exams

[6] Iziraa – Kisimiri Secondary School former national champion continues to impress (2024 perspective)

Zaidi ya Matokeo ya Ujifunzaji: Thamani Iliyojengeka

Mwalimu Kisongo alisukuma mipaka ya mafanikio kuwa ni zaidi ya alama za darasani. Alisisitiza kuwa maadili, mienendo na stadi za maisha ni sehemu muhimu ya elimu bora. Chini ya uongozi wake, malezi na tabia njema vilikuwa ni sehemu ya utamaduni wa shule, kuhakikisha kuwa hili halipimwi kwa kuwa na matokeo ya masomo tu, bali pia kwa tabia. Hata pamoja na kuendelea kufanya vizuri kitaaluma, Mwalimu Kisongo aliendelea kusisitiza zaidi.

"Tuna uhakika wa kidato cha sita kupata daraja la Kwanza kwa urahisi. Lakini ina umuhimu gani kama hawatakuwa na tabia na maadili mazuri?"

Chakujifunza katika Utawala wa shule

Kwa viongozi wa elimu sikuhizi, Mwalimu Kisongo anatoa ushauri:

- **ua kwanini unaongoza.** "Jua kwanini wewe ni mkuu wa shule."
- **Miliki matokeo.** "Kocha anawajibika kwa matokeo."
- **Endelea kujifunza wakati wote.** "Ili uendelee kuwa mbunifu wa mabadiliko."

Makala hii ya Mwalimu Kisongo, inatoa elimu kwa viongozi wa elimu wote:

- **Uongozi unaomlenga mwanafunzi** unaweza kuzipa nguvu hata taasisi zilizo dhaifu zaidi.
- **Uvumilivu na uwajibikaji** ni muhimu katika mazingira ambayo walimu wanaweza kuanza kwa kupinga mabadiliko.
- **Uongozi wa kubadilisha mifumo** unaunganisha matokeo yanayopimika na maadili, na kujenga taasisi endelevu hata baada ya kiongozi mmoja kuondoka.
- **Falsafa binafsi ya uongozi**—kujua kwa nini unaongoza, kumiliki matokeo, na kujitolea kujifunza maisha yote—ni muhimu kwa mabadiliko ya kimfumo.

Kwanini Makala ya Mwalimu Kisongo's ni Muhimu

Makala hii inaonesha jinsi uongozi unaoongozwa na maadili, jumuishi na unaolenga matokeo unaweza kuibadilisha taasisi iliyokuwa ikidorora na kuigeuza kuwa kinara wa kitaifa. Unaonesha nguvu ya kiongozi katika kuweka mifumo ya kudumu, usawa, na maendeleo katika nyaja zote. Safari ya Kisimiri chini ya Mwalimu Kisongo inaonyesha kuwa hata katika mazingira yenye upungufu wa rasilimali na yaliyoko vijijini, uongozi wa kubadilisha mifumo unaweza kuleta mabadiliko ya kudumu yanayotambuliwa kitaifa.